

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

Simu: 025-2540035/7  
Barua pepe: [ded@kyeladc.go.tz](mailto:ded@kyeladc.go.tz)  
Nukushi: 025-2540425



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)  
S. L. P. 320, KYELA,  
MBEYA – TANZANIA

Tarehe 17.09.2019

Kumb. Na. KDC U.4/ 1 VOL.2/02

## TANGAZO LA NAFASI YA AJIRA YA MUDA YA UANDIKISHAJI NA UANDAaji WA ORODHA YA WAPIGA KURA

*(Limetolewa chini ya Kanuni ya 10 ya kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa Halmashauri ya kijiji na Mwenyekiti wa kitongoji Tangazo la Serikali Na. 373 la tarehe 26.04.2019)*

Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela anapenda kutangaza nafasi 408 za ajira ya muda ya uandikishaji na Uandaaji wa Orodha ya Wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika tarehe 24.11.2019

### 1. Sifa za Mwombaji

- (1) Awe mtumishi wa Umma,
- (2) Awe mwadilifu, mchapakazi na mtendaji haki,
- (3) Asiwe na dhamana/uongozi katika /chama chochote cha Siasa
- (4) Asiwe Mtendaji wa Kijiji au Mtendaji wa kata

### 2. Majukumu/Kazi atakazofanya

- (1) Kuandikisha na kuandaa orodha ya wapiga kura kwa kutumia fomu maalum itakayotolewa na msimamizi wa Uchaguzi. Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku saba kuanzia tarehe 08.10.2019 hadi 14.10.2019 – saa 2.00 asubuhi hadi saa 12.00 Jioni.
- (2) Kubandika nakala ya Orodha ya wapiga kura kwenye sehemu ya matangazo ya Uchaguzi siku moja baada ya zoezi la uandikishaji kukamilika, yaani tarehe 15.10.2019.
- (3) Kutunza nakala halisi (Original) ya Orodha ya wapiga kura na kuwasilisha kwa msimamizi wa Uchaguz, na

- (3) Kuwa tayari kutekeleza kwa wakati maelekezo mengine yote Yatakayotolewa na msimamizi wa uchaguzi kuhusiana na zoezi la uandikishaji na uandaaji wa Orodha ya wapiga kura.

**3. Masharti ya Jumla**

- (1) Mwombaji awe mkazi wa kata anayoomba kuandikisha wapiga kura  
(2) Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji mwenyewe na yapitishwe na Mtendaji wa Kata kwa uthibitisho.

- (3) Maombi yote yaandikwe kwenda kwa :-

**Msimamizi wa Uchaguzi**

**Uchaguzi wa Serikali za Mitaa**

**Halmashauri ya Wilaya ya Kyela**

**S.L.P. 320 – KYELA.**

- (4) Barua zote za maombi ziwasilishwe kwa Mtendaji wa Kata ili yeye azipitishwe, azikusanye na kisha aziwasilishwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi

- (5) Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 27.09.2019 siku ya Ijuma – saa 9.30 Alasiri.

Tangazo hili limetolewa na:



**Benedict M. Missani**

**Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa**

**Halmashauri ya Wilaya ya Kyela**